

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR  
BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR  
MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

102

KISWAHILI

MUDA: SAA 2.30

JUMATANO 01 NOVEMBA, 2023 MCHANA

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MANNE (4) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
11.		
12.		
JUMLA		
SAINI YA MHAIKIKI		



023102706

Mtihani huu una kurasa 12 zenye maandishi

**SEHEMU A: (Alama 15)**

**UFAHAMU**

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

**1. Soma habari hii kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.**

Siku moja Sudi aliondoka na wasaidizi wake kwenda kuvua. Wanunuzi walisubiri arudi na samaki ili wapate kitoweo. Siku hiyo bila ya kutarajia Sudi hakuonekana. Usiku ulipoingia, vijana na wazee mitaani wakaanza kupata wasiwasi. Waliamua kufunga safari kwenda kumfuatilia pwani.

Kikundi cha vijana kilikuwa pwani ili kupata kujua kulikoni. Walipofika pwani waliona watu wengi wamekusanyika wakiangalia kwa mshangao. Walikuwa na shauku kujua kulikuwa na nini. Walipokaribia walimuona Sudi na wasaidizi wake wamelala chini wakitweta. Wananchi walishirikiana kuwapa huduma ya kwanza.

Baada ya muda Sudi na wenzake walipata nafuu. Walipoulizwa matatizo yaliyowapata Sudi alieleza. "Tumekumbwa na dhoruba kali" Alisema kuwa asubuhi walipoanza safari, bahari ilikuwa shwari, walipofika katikati ya bahari, mvua ndogondogo ilianza kunyesha. Hali hii haikuwapa mashaka yoyote, walijua kuwa hali ile ilikuwa ni ya kawaida baharini. Lakini ghafla upepo mkali ulianza kuvuma, umwesa mkali ulionekana kila pembe na radi kunguruma. Bahari ilikuwa na mawimbi makubwa siku hiyo na dau lao lilianza kwenda mrama. Tanga liliruka na dau likakwama kwenye mwamba. Sudi na wenzake walijua kuwa walikuwa kwenye matatizo ambayo yangegharimu uhai wao.

Haraka haraka walitweka tanga la hakiba na kuelekea kwenye kisiwa cha karibu. Maji yalianza kuingia katika chombo chao. Kumbe chombo kilikuwa kimepata ufa. Mara waliona mwamba mwingine, wakaukwepa hawakukubali kufa kikondoo, wakapania kupigana kiume ili kuokoa maisha yao.

Sudi na wenzake walipangiana zamu za kutoa maji chomboni. Wengine walikuwa hawana vyombo vikubwa vya kutekea maji. Kwa hiyo walitumia birika walilokuwa wamebebea maji ya kunywa. Kazi hii iliwachosha sana kwa sababu maji yaliingia kwa kasi na dau lilianza kuzama.

Hata hivyo, hawakukata tamaa. Mara waliuona mtumbwi kwa mbali. Mtumbwi huo ulikuwa unafanya msako wa kuwatafuta. Sudi na wenzake walipepea mashati yao ili waweze kuonekana mahali walipokuwa. Mtumbwi uliwasogelea na kuwachukuwa.

**MASWALI**

- a) Eleza sababu iliyowafanya Sudi na wenzake kuchelewa kurudi baharini.

---

---

---

- b) Sudi na wenzake walikuwa wakifanya kazi gani?

---

---

---

- c) Dau la kina Sudi lilipatwa na nini baada ya kwenda mrama?

---

---

---

- d) Bainisha mbinu aliyoitumia Sudi na wenzake ili kukabiliana na maji yaliyokuwa yakiingia katika chombo chao.

---

---

---

- e) Taja ishara waliyoionesha Sudi na wenzake ili kujulikana kwa urahisi mahali walipo.

---

---

---

2. Fupisha aya ya tatu (3) ya habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi ishirini (20).

---

---

---

---

---

**SEHEMU B: (Alama 40)**

**SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

**Jibu maswali MANNE (4) katika sehemu hii.**

3. Badilisha sentensi zifuatazo kwenda katika kauli ya kutendwa.

a) Paka anakunywa maziwa.

\_\_\_\_\_

b) Fundi alishona viatu vyako.

\_\_\_\_\_

c) Kamaria amekichana kitabu changu.

\_\_\_\_\_

d) Wakulima watawuna mazao mengi mwaka huu.

\_\_\_\_\_

e) Babu amewasha moto.

\_\_\_\_\_

4. a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo.

i. Nomino

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

ii. Kiunganishi

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

iii. Sentensi

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

## Nambari ya Mtahiniwa \_\_\_\_\_

b) Unda sentensi ambatano kwa kutumia sentensi zifuatazo.

i. Yeye amejifunza sarufi. Mimi nimejifunza fasihi.

---

---

---

ii. Wanafunzi waliofanya vizuri wamepewa zawadi. Wanafunzi waliofeli wamerudia darasa.

---

---

---

5. a) Eleza dhima tatu (3) za lugha kisiasa.

i. 

---

---

ii. 

---

---

iii. 

---

---

b) Ziandike nambari zifuatazo kwa kuzingatia alama na vituo.

i. 64967

---

ii. 2338512

---

6. a) Tafsiri aya ifuatayo kwa Kiswahili.

I am a student. My father is a doctor and my mother is a teacher. At home I live with my father. I have a white cat at home whose name is Hellen. I love my cat very much. I prepare some milk and some fish for Hellen every morning.

---

---

---

---

- b) Eleza tofauti iliyopo kati ya kidahizo na kitomeo.

---

---

---

---

---

---

7. a) Eleza michango mitatu (3) ya njia za kisasa za mawasiliano katika kuleta maendeleo ya Zanzibar.

i. 

---

---

ii. 

---

---

iii. 

---

---

- b) Taja faida mbili (2) za lahaja za Zanzibar.

i. 

---

---

ii. 

---

---

**SEHEMU C: (Alama 30)**

**FASIHI**

**Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii.**

8. a) Nini maana ya mashairi?

---

---

---

---

---

---

- b) Tunga beti nne (4) za shairi linalozungumzia athari za kuporomoka kwa maadili ya kizanzibari.

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

9. Lete maana ya methali zifuatazo.

i. Mcheza kwao hutunzwa.

---

---

---

ii. Usiache mbachao kwa msala upitao.

---

---

---

iii. Pilipili usiyoila inakuwashia nini?

---

---

---

iv. Hamadi kibindoni silaha mkononi.

---

---

---

v. Fadhila za punda ni mateke.

---

---

---



10. a) Eleza kwa ufupi dhana ya hadithi fupi.

---

---

---

---

b) Andika sifa tano (5) za hadithi fupi.

i. \_\_\_\_\_

ii. \_\_\_\_\_

iii. \_\_\_\_\_

iv. \_\_\_\_\_

v. \_\_\_\_\_

c) Eleza dhima tano (5) za hadithi fupi.

i. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

ii. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

iii. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

iv. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

v. \_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

**Nambari ya Mtahiniwa** \_\_\_\_\_

**SEHEMU D: (Alama 15)**

## UTUNGAJI

**Jibu swali MOJA (1) katika sehemu hii.**

11. Andika Insha isiyopungua maneno 120 na isiyozidi maneno 150 yenye kichwa cha habari "Ajali za Barabarani".

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

12. Andaa tangazo la biashara ya nguo za kitoto kwa njia ya gazeti.

This image shows a blank sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.







